

ASILIMIA 97 YA WATOTO MKOANI SHINYANGA WAMEPATIWA VYETI VYA KUZALIWA BURE.

Watendaji wa Wilaya na Halmashauri zote za Mkoa wa shinyanga wameagizwa kuongeza kasi na ufuatiliaji wa karibu wa Mpango wa usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watoto wenye umri chini ya miaka mitano ili kufikia lengo la Mkoa huo la kuwapatia vyeti vya kuzaliwa Watoto wote kwa kipindi cha miezi mitatu badala ya sita.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe Zainab Telack katika kikao cha tathmini kuhusu Maendeleo ya Mpango wa Usajili wa Watoto walio na Umri Chini ya Miaka Mitano unaotekelezwa katika mkoa huo.

“Ahadi yetu kama Mkoa tumeitekeleza kikamilifu kwa kuweza kusajili watoto 304,002 kati watoto 314,540 ambao ni sawa na asilimia 97 ya watoto wanaoishi katika Mkoa wetu na kazi hii kubwa imefanyika ndani ya miezi miwili ambapo kabla ya hapo ni asilimia 9.4 tu ndio walikuwa na vyeti vya kuzaliwa” Alisema Mhe. Telack

Katika hotuba yake Mkuu wa Mkoa amesisitiza kuwa Serikali ya awamu ya tano imedhamiria kwa dhati kufanya maboresho katika maisha ya wananchi kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii karibu na maeneo wanakoishi Wananchi kama walivyofanya RITA kwa sasa usajili wa Watoto chini ya umri wa miaka mitano kufanyika katika ngazi ya kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya mama na Mtoto.

Kwa upande wake Kaimu afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson amesema RITA wanaendelea na kufanya maboresho zaidi ya huduma zake pamoja na mifumo ya TEHAMA ambapo Mkoa wa shinyanga ni miongoni mwa Mikoa iliyochaguliwa kufanya majaribio ya Kitaifa ya mfumo mpya wa usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambapo watoto zaidi ya muri wa miaka mitano(5) hadi kumi na saba (17) na wale watakozaliwa watasajiliwa na kupatiwa cheti cha kuzaliwa kwa mfumo wa Kompyuta katika vituo vitakavyoainishwa ngazi ya kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya mama na Mtoto.

Bi Hudson ameongeza kuwa katika tathimini ya Mpango wa usajili na kuwapatia vyeti vya kuzaliwa Watoto wenye umri chini ya miaka mitano wa Mkoa wa Shinyanga wamegundua kuwa kuna haja ya kuanza mapema utekelezaji wa mfumo mpya ta TEHAMA unaojulikana kama BRS4G ili kumaliza kabisa makundi mengine ya Wananchi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa kwa kuweka mifumo thabiti itakayoweka uhakika wa ukusanyaji wa takwimu sahihi na kwa wakati ambapo kwa sasa vifaa vyote vinavyohitajika vimeshatawanywa na tayari kwa kuanza majaribio hayo.

Wakati huohuo wito umetolewa kwa Taasisi zote za Serikali kuwasiliana na RITA pindi wanapokuwa na wasisi juu ya uhalali wa cheti cha kuzaliwa cha Mwananchi yeyote wanayemtilia mashaka badala ya utaratibu uliopo hivi sasa kwa Taasisi hizo kukataa kupokea aina fulani ya vyeti bila ya sababu za msingi na hivyo kusababisha usumbufu kwa wananchi na Mamlaka nyingine za Serikali hivyo kurudisha nyuma jitihada zinazofanyika za kuwasajili na kuwapatia vyeti vya kuzaliwa Watoto wenye umri chini ya miaka mitano.